



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 1**  
**SWAHILI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Tuesday 3 May 2005 (morning)  
Mardi 3 mai 2005 (matin)  
Martes 3 de mayo de 2005 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento.

Toa maoni yako juu ya **moja** ya tungo zifwatazo.

1. (a)

	Ewe uliye na maya Ina matata duniya Mpaka umeondoa	shauri langu lishike kwa kudumu ndani yake huzuni yako ucheke
5	Cheka cheko ni furaha Cheka upone jaraha Na mwili kupata siha	uache kusikitika yaepuke na mashaka ukianguka inuka
	Inuka juu inuka Inuka na kesho cheka Endelea na kucheka	chini usigaegae kucheza uendele kwa shangwe kuu na yowe
10	Cheko iwe maridhawa Mungu muuba dunia Huzuni itakimbia	kunjua uso ucheke furaha mchezo wake kicheko ni dawa yake
15	Tena fanya kila siku Na mchana na usiku Acha msiba kushuku	kicheko kifutulize furaha iendeleze kukujia jikataze
	Cheka na watu kukicha Ucheke jua likichwa Huzuni yako kuacha	na usiku ukariri na kisha uwe tayari kwa sababu huhasiri
20	Cheka sasa kwa furaha Dhiki ni kama mzaha Haya cheka ha, ha, ha	dhiki ingawa usoni asiyecheka ni nani? ndiyo ada duniani
	Cheka mwanadamu cheka Msiba kwake dhihaka Ni mwenzake wa kuweka	mtu kaumbwa acheke kicheko mtu mwenzake huzuni adui yake
25	Msiba unazeesha Ndiyo sumu ya maisha Mwilini inaozesha	mtu bado ni mchanga inafaa kujitenga uzikwe chini ya changa
30	Cheka uzuwie kwisha Furaha ndiyo tamasha Hata nyota zakumbusha	maishayo mbiombio kiumbe aliyonayo kuwa nazo hali hiyo

Kutoka: *Kusanyiko la Mashairi*, Ali A. Jahadhmy, 1977

1. (b)

- Kila siku asubuhi hugombana na mke wangu. Sababu? Hataki kunisafishia viatu vyangu. Si neno kama ningekuwa nafanya kazi ya ukulima au ya ujenzi au ya kuchimba mitaro na mahandaki. Lakini nimesadifu kuwa na kazi ya ofisini, na Nairobi usafi na umaridadi wa mtu huanza miguuni tena ukapanda surualini hadi kwenye shati, koti, tai na sigara. Hiyo tai ndiyo fadhili, japo ukosi wa shati ni mchafu. Usoni haidhuru, kwani ukionyesha ishara ya matongotongo ofisini, mwenzako aweza kukuzindua na ukapeleka kidole machoni na kuyafuta, au unaweza kujitapa, “Ah, faida ya kuchelewa kulala. Jana nilikwenda *party* Lavington, sijarejea nyumbani mpaka saa kumi alfajiri. Hivyo leo nimeamka saa mbili!” Nywele haziulizwi, maana kila mtu ana shoo yake. Mdomo ndiyo kabisa.
- 5
- 10 Basi hasira zangu juu ya mama watoto hunifanya kila siku nitoke ofisi kiasi saa nne. Hutoa dharura ya kwenda Benki au posta au kulipa bili ya taa – dharura hazishi kwa anayezitafuta – tena hunyoosha mpaka mkahawani kupasha tumbo moto. Siku nyingine huenda “Rendezvous” au “Currypot”. Yote hutegemea suti niliyovaa. Nikishapata kikombe cha kahawa na “sandwich” moja hukumbuka ugomvi wangu na mzee-chema nikafululiza mpaka “Portal Street” kwa Kingo. Kingo ni mtiaji rangi viatu. Ndiyo amali yake miaka nenda miaka rudi. Ilivyokuwa mimi huonana naye takriban kila siku sasa miaka mitatu, baina ya saa nne na nusu na tano kasorobo, tumepata kujuana hadi binadamu wanavyoweza kujuana. Tumeambiana mengi. Nyingine siri za watu amenipa siwezi kuziandika. Mengine ni mambo ya dakhalia yanyohusu viongozi na watu wenye vyeo hapa mjini. Baadhi yanahusu usalama wa nchi. Lakini nitajaribu kudokoa kidogo vile vichupuchupu
- 15
- 20 kwa manufaa ya wasomaji. Basi mikasa inayofuata ni baadhi ya mambo anayonizungumzia. Hao watu anaowajua, wachache nawafahamu na wengine siwafahamu. Bila ya shaka imenilazimu kuyachambua maneno ya Kingo na kuyabadilisha hapa na pale ili yaweze kuandikika vyema, kwani kama ilivyo desturi ya wazungumzaji wa sifa, hawasemi moja likesha, bali huruka hapa na pale, na kutumia methali, vijembe na mafumbo ambayo yakiandikwa safi bila ya kuchujwa hayaleti
- 25
- maana yoyote. Ndiyo tofauti baina ya kudaka kauli motomoto inapotoka kinywani – mvuke wa mate na pumzi ungali mvukute – na kuangaza mistari meusi juu ya karatasi.

Kutoka: *Pepeta*, S.S. Yahya, 1973